

**BENKI KUU YA TANZANIA**  
16 Barabara ya Jakaya Kikwete  
S. L. P. 2303  
40184 DODOMA  
**TANZANIA**

Simu: +255 22 223 3167  
Barua Pepe: [botcommunications@bot.go.tz](mailto:botcommunications@bot.go.tz)



**BANK OF TANZANIA**  
16 Jakaya Kikwete Road  
P.O. Box 2303  
40184 DODOMA  
**TANZANIA**

Phone: +255 22 223 3167  
Email: [botcommunications@bot.go.tz](mailto:botcommunications@bot.go.tz)

**29 Desemba 2023**

## **TAARIFA KWA UMMA**

### **HUDUMA YA UPOKEAJI WA SARAFU ZISIZOTUMIKA KWA MUDA MREFU KATIKA OFISI ZA BENKI KUU YA TANZANIA NA BENKI ZA BIASHARA**

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuufahamisha Umma kwamba huduma ya kupokea sarafu (coin) zilizotunzwa kwa muda mrefu bila kutumika itatolewa kwa wananchi wote au taasisi ili kubadilishwa na noti. Huduma hiyo itatolewa katika ofisi zote za Benki Kuu pamoja na benki za biashara nchini. Hatua hii imechukuliwa kutokana na utafiti uliobaini kuwepo kwa sarafu nyingi za shilingi 200, 100, na 50 ambazo hazitumiki kwa muda mrefu katika mzunguko wa kiuchumi na badala yake zimetunzwa au kuwekwa nyumbani, ofisini, kwenye magari, biashara na taasisi mbalimbali nchini.

Huduma hii itatolewa kama zoezi maalumu la mwezi mmoja kuanzia tarehe 2 Januari 2024 ili kuendelea kulinda ubora wa sarafu zetu dhidi ya uharibifu unaotokea katika mazingira yasiyokuwa salama na kurejesha fedha hizo kwenye mzunguko wa kiuchumi. Hivyo, wananchi wote wenyе sarafu (coin) za shilingi 200, 100 na 50 ambazo zimetunzwa bila kutumika kwa muda mrefu na wangependa kuzibadilisha ili kupata noti au kuzitunza kama amana katika akaunti zao, wanaombwa kuziwasilisha kwenye ofisi za Benki Kuu au benki za biashara kwa ajili ya kupata huduma hiyo.

Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana na Bw. Ilulu S. Ilulu, simu Na. 0745802007 au tumia barua pepe: [info@bot.go.tz](mailto:info@bot.go.tz) au [botcommunications@bot.go.tz](mailto:botcommunications@bot.go.tz)

A handwritten signature in blue ink, appearing to read "Emmanuel M. Tutuba".

**EMMANUEL M. TUTUBA**  
**GAVANA**  
**BENKI KUU YA TANZANIA**